JARIDA LA SINGIDA RS

TOLEO LA MWEZI OKTOBA,2024

RC DENDEGO Ashiriki zoezi la uandikishaji daftari la wapiga kura, Uchaguzi Serikali za Mitaa 2024

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, Octoba 11, 2024 ameonyesha mfano bora wa uongozi kwa kujiandikisha kwenye orodha ya wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, 2024

Zoezi hilo limefanyika katika kituo cha kujindikisha cha Shule ya Msingi Sababasaba, kata ya Utemini Singida Mjini

RC. Dendego, ameelezea tofauti kati ya zoezi lililopita la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na hili la Daftari la Wakazi, akisisitiza umuhimu wa uandikishaji huu kwa ajili

ya uchaguzi wa wenyeviti wa mitaa na wajumbe wa kamati za mitaa, pamoja na viongozi wa vijiji na vitongoji

"Hili ni zoezi tofauti na lile lililopita. Ikiwa hujajiandikisha hutoweza kumpigia kura kiongozi unayemtaka katika mtaa wako". Amesema RC Dendego

Katika mwendelezo wa zoezi hilo, Mkuu wa mkoa huyo amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi ili kujiorodhesha katika Daftari la Wakazi, ili waweze kuwachagua viongozi wanaowafaa katika maeneo yao huku akihimiza kila mmoja kuzingatia wajibu wake wa kisiasa akisisitiza kwamba sauti ya wananchi ni muhimu katika mchakato wa uchaguzi

Zoezi hili lina umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kuwa viongozi wanaoingia madarakani wanachaguliwa kwa njia ya haki na uwazi na kwamba kila raia anapata fursa ya kushiriki katika mchakato wa kisiasa

Kongamano la Wanawake na Uchaguzi lafana mkoani Singida

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewahimiza wanawake mkoani Singida kujitokeza kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, 2024 na uchaguzi mkuu wa mwakani 2025 ili waweze kuwa na nafasi ya kushiriki katika ngazi za maamuzi

Amesema hayo Oktoba 9,2024 wakati akifungua kongamano la wanawake na uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 ambalo linawashirikisha wanawake kutoka wilaya zote za mkoa huu lengo likiwa ni kuwahamasisha kujitokeza kushiriki uchaguzi mwaka huu na mwakani huku sambamba na kampeni za uchaguzi zitakazonza rasmi 20 hadi 26 Novemba 2024 huku akiviomba vyama vyote vya siasa vitakavyoweka wagombea kufanya kampeni za kistaarabu kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo

"Nitumie nafasi hii kuwakumbusha kwamba 27 Novemba, 2024 ni siku ya uchaguzi wa Viongozi wetu wa Serikali za Mitaa (Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji) nchi nzima, Kaulimbiu ya uchaguzi huu inasema "Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo ya Taifa letu, maandalizi yote ya kufanikisha uchaguzi huu yamekamilika kwa kuanza na zoezi la uandikishaji wa wapiga kura lililofanyika kuanzia tarehe 25 Septemba, 2024 hadi tarehe 01 Oktoba, 2024,"amesema Dendego

Mheshimiwa Dendego amesema takwimu za wamawake mkoani Singida haziridhishi kwani pamoja na mkoa kuwa na idadi kubwa ya wanawake lakini wenyeviti wanawake ni 96 tu, mitaa ipo 53 wenyeviti Wanawake wapo 03 tu na jumla ya Wanawake katika nafasi ya ujumbe wa Serikali katika ngazi zote

Siku 10 za kuhamashisha Wananchi kujiandikisha katika Daftari la Mpiga Kura

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, ameongoza timu operesheni ya kuwahamasisha wananchi kujitokeza katika vituo maalum vilivyoandaliwa katika maeneo yao ya makazi kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, 2024

Zoezi hili limeanza Octoba 11 hadi mwezi Octoba 20, 2024

Ikungi yaibuka vinara kanda ya kati mbio za mwenge wa uhuru

WILAYA ya Ikungi mkoani Singida imeibuka mshindi wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2024 kwa Kanda ya Tatu, na kuweza kukabidhiwa kikombe na fedha sh. milioni moja,wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa huo Halima Dendego

Ikungi imeshinda kwenye Kanda ya Tatu yenye mikoa ya Ruvuma, Singida, Dodoma, Manyara, Kagera na Mara, ikiwa ni ishara kuwa walikidhi vigezo kuanzia mapokezi ya Mwenge wa Uhuru, hamasa, na ubora wa miradi ikiwemo miradi kuakisi thamani ya fedha, na kuwepo kwa vielelezo vyote vya manunuzi na vifaa

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Justice Kijazi, alisema ushindi huo ni wa wananchi wa Wilaya ya Ikungi na mkoa wote wa Singida, na imewapata moyo kuweza kuendelea kufanya vizuri katika utekelezaji wa miradi

Kijazi amesema wao kama viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia shughuli za maendeleo ikiwemo miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu,

Wanawake elfu 3 kushiriki Tamasha la Uchaguzi Serikali za Mitaa Singida

Mkoa wa Singida umeandaa tamasha kubwa litakalo washirikisha wanawake zaidi ya 3,000 kutoka wilaya zote za mkoa huu lililobeba jina la Wanawake na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, akizungumza Oktoba 7, 2024 na waandishi wa habari, amesema tamasha hilo litafanyika Oktoba 10, mwaka huu kwenye viwanja vya Bombadia vilivyopo Manispaa ya Singida

Amesema Spika wa Bunge mstaafu ambaye pia ni Kamisaa wa Sensa nchini, Anne Makinda, atakuwa mgeni rasmi katika tamasha hilo ambalo lengo lake ni kuwahamashisha wanawake kushiriki katika uchahuzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 27, 2024

"Serikali yetu bora na sikivu chini ya uongozi wa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, imeweka taratibu mbalimbali za kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata taarifa sahihi za uchaguzi na anahamasishwa ili aweze kushiriki katika uchaguzi na hivyo kutimiza haki yao ya kikatiba, hivyo tamasha

hili ni moja ya mipango ya mkoa katika kuwafikia wananchi wengi hasa makundi maalum ya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu," amesema Dendego

Dendego amesema tamasha hilo ni fursa kubwa na ya kipekee kwa wanawake wa Mkoa wa Singida kushiriki pamoja na mama Anne Makinda ambaye ni kiongozi mbobezi ili waweze kupata ladha sahihi ya wanawake na uongozi na matumizi ya takwimu katika kufanya maamuzi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo

"Kongamano letu litahusisha wanawake takribani 3,000 kutoka wilaya zote tano za Mkoa wa Singida na kubwa zaidi wanawake hawa vinara wanatoka kwenye ngazi za chini kabisa kwa maana ya vijiji mitaa na kata," amesema Dendego

Ameongeza kuwa lengo la kuwakutanisha wanawake hao ni kuwahabarisha na kuwahamasisha kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa,uchaguzi ambao unatoa viongozi watakaosimamia maisha yao ya kila siku

"Pamoja na tamasha hili,bado kuna mikutano mbalimbali inaendelea mabonanza ya michezo yanaendelea na ziara za viongozi nazo zinaendelea, lengo ni kiwafikia wananchi walio wengi na hasa maeneo ya pembezoni na kuwaleta pamoja kwenye jambo hili kubwa katika nchi yetu," amesema Dendego

Aidha, amesema tamasha hili mbali na kuwaleta pamoja wanawake vinara litaanbatana na taarifa fupi za maendeleo na uzinduzi wa mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia na litasindikizwa na burudani kutoka kwa wasanii mahiri.

RC DENDEGO aziagiza Halmashauri kufikisha fursa Mikopo ya 10% kwa walengwa mpaka vijijini

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego, ameagiza Halmashauri zote mkoani humo kuhakikisha mikopo ya asilimia 10 inawafikia walengwa hadi vijijini ikiwa ni pamoja na akina mama, vijana, watu wenye ulemavu, na wazee ili kuimarisha uchumi wa wananchi na kusaidia maendeleo hadi ngazi za vijiji

RC Dendego ametoa agizo hilo kwenye mkutano wa Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi **"Imarisha Uchumi Na Mama Samia"** (IMASA)" iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano RC Social uliyopo Singida Mjini Octoba 3, 2024

Mkuu wa Mkoa huyo, amewataka vijana kuachana na tabia ya kutumia muda wao kwenye michezo ya pool table na badala yake wachangamkie fursa zinazotolewa na mifuko ya uwezeshaji kiuchumi pamoja na mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri, ili waweze kujikwamua kiuchumi

RC Dendego, amewasisitizia wakinamama na walezi kutowakumbatia vijana wenye umri wa zaidi ya miaka 18 ambao bado wanakaa nyumbani bila kujishughulisha akieleza kuwa wengi wao hupelekea kujihusisha na vitendo vya uhalifu

Kwaupande wake, Katibu Tawala Mkoa wa Singida Dkt. Fatuma Mganga, amepongeza na kumshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia mikopo ya asilimia 10 kupatiwa makundi ya akinamama, vijana, watu wenye ulemavu na wazee huku akiwataka kutumia fursa za mikopo hiyo kwenda kuanzisha viwanda vidogo vya uzalishaji nishati mbadala akisisitiza kuwa hatua hii itachangia katika kukuza uchumi wa mkoa na kuboresha maisha ya wananchi

Ameeleza kuwa nishati mbadala ni muhimu katika kuimarisha maendeleo endelevu na kupunguza utegemezi wa nishati ya kawaida.

"Singida tumezikataa changamoto za wanawake" RC Dendego

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe Halima Dendego amewahamasisha wanawake kujiandikisha katika daftari la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, 2024 na kugombea nafasi za uongozi ili wanawake kuwa na nafasi ya kutoa maamuzi pale yanapoja iliwa maswala mbalimbali ya maendeleo

Hayo yamesemwa hii leo tarehe 16 Octoba, 2024 katika maadhimisho ya kimataifa ya mwanamke wa kijijini yalioanzishwa kwa mara ya kwanza na baraza kuu la umoja wa mataifa mwaka 2007 kupitia azimio maalumu la kutambua jukumu na mchango wa wanawake wa Vijijini katika kuimarisha maendeleo ya Kilimo maendeleo ya vijiji kuboresha usalama wa chakula na kutokomeza umasikini ambayo yemefanyika ukumbi wa shule ya sekondari Ikungi

Mkuu wa Mkoa amesema kuwa nafasi hizi za uongozi zimewekwa ili wanawake wapaze sauti katika yale ambayo yamekuwa ni kero na yanakwamisha maendeleo ya wanawake kiuchumi na nyanja zingine zote

"Singida hususani Wilaya ya Ikungi tumeshaanza kuzikataa changamoto za wanawake tunasema tutakapolima tupewe nafasi ya maamuzi kipi kiuzwe na kipi kibaki kwa ajili ya chakula" amesema mkuu wa Mkoa

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ikungi Mhe Thomas Apson ameongeza na kusema kuwa ipo haja pia wanawake kuwaheshimu waume zao ili kuondokana na migogoro ya mara kwa mara inayojitokeza na kupeleke mifarakano katika familia

"Nimejifunza hilo kwenye mikutano yangu ya kusikiliza kero za wananchi inapofika saa 12 wanawake wanawahi nyumbani kuwapikia waume zao huu ni Utamaduni mzuri tusiige tamaduni mbaya" ameongeza Mkuu wa Wilaya

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Ndg. Richard Rwehumbiza akisoma taarifa mbele ya Mgeni Rasmi kuwa maadhimisho haya hufanyika kila mwaka ili kuelimisha jamii kuhusu jitihada mbali mbali zinazofanyika na serikali na asasi mbalimbali kukuza uchumi na mshikamano wa wanawake nchini na duniani kote

Naye Afisa Maendeleo ya jamii Bi Haika Massawe mara baada ya maada mbalimbali kujadiliwa juu ya mwanamke wa kijijini ametaja baadhi ya maazimio ambayo kwa kushirikiana na wanawake wa Wilaya ya Ikungi yatatekelezwa kubwa ikiwa ni pamoja na utoaji kwa wakati mikopo ya asilimia 10 za halmashauri na kufatilia utendaji wao wa kazi ili kurejesha mikopo hiyo kwa wakati na mengine ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi kutatua changamoto zao kama kugombea nafasi za uongozi na kujumuika katika kutoa maamuzi

"Tengeni Bajeti za kuhudumia Elimu ya watu wazima na Elimu nje ya Mfumo rasmi"

Haya yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Mhe Dkt Vincent Mashinji akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe Halima Dendego wakati wa Maadhimisho ya Juma la Elimu ya watu wazima na Elimu nje ya Mfumo yaliyofanyika tarehe 01 Oktoba 2024 Kata ya Chikuyu Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni

"Tengeni Bajeti za Kuhudumia Elimu ya watu wazima na Elimu nje ya Mfumo rasmi Ili kuwezesha na kuhakikisha wenye mahitaji ya Elimu hii kuipata, Lakini pia wekeni mikakati ya kudhibiti changamoto za Elimu ya watu wazima na Elimu nje ya Mfumo"

Sambamba na Hilo Mhe Dkt Mashinji amepongeza jitihada zinazofanywa na Idara ya Elimu Mkoa wa Singida kwa kuandaa Maadhimisho haya lakini pia kusimamia Elimu hii ya watu wazima na Elimu nje ya Mfumo kuendelea kuwepo na kusaidia wengi katika Mkoa wa Singida

"Tumepita Mabanda ya Maonesho tumeona namna Elimu hii ya watu wazima na Elimu nje ya Mfumo ilivyosaidia wengi katika Mkoa wetu wa Singida hivyo niwapongeze sana sana kwa Kazi nzuri"

Vile vile Dkt Mashinji amewahamasisha na kuwasisitiza Wananchi kushiriki zoezi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu 2024

"Kupitia hadhara hii napenda kuwakumbusha na kuwasisitiza kushiriki zoezi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuanzia tarehe 11- 20 oktoba tutakua na zoezi la kujiorodhesha kwenye daftari la mpiga kura na tarehe 27 Novemba ndio Siku ya Uchaguzi, hivyo niwaombe sana wananchi wenye Sifa za kugombea na kupiga kura tushiriki mazoezi haya kikamilifu

Mkesha wa Mwenge wafana, Singida yang'ara Mbio za Mwenge Kitaifa

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe.Halima Dendego amesema wananchi wataendelea kuuenzi, kuheshimu na kutekeleza kwa vitendo ujumbe unao ambatana na mbio za mwenge wa uhuru ili kuchochea maendeleo ya wanasingida

Mhe. Dendego amesema

hayo jana usiku katika viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wakati wa hafla ya mkesha wa mwenge wa uhuru ukitokea Jijini Mwanza kuelekea Mlima Kilimanjaro

"Mkoa unatambua kazi kubwa inayofanywa na mbio za mwenge wa uhuru ikiwa ni pamoja na kudumisha amani na mshikamano sambamba na kuhamasisha maendeleo,toka ulipowashwa mwezi wa nne mwaka huu na kuzunguka mikoa yote ya Tanzania Bara na visiwani mwenge umeendelea kuwaimarisha watanzania"

Akiahidi kuendelea kusimamia yale yote yaliyokuwa yanahimizwa na ujumbe wa mbio za mwenge amesema wanasingida wana bahati kwa kuwa mwenge umelala mkoani humo wakati zoezi la wananchi kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa likiendelea

Dendego amemponge-za Rais Dr Samia Suluhu Hasan kwa kuuteua Mkoa wa Singida kuwa sehemu ya kusindikiza Mwenge wa uhuru kuelekea mlima Kilimanjaro kwa kuwa hilo ni tukio linalobeba ujumbe mzito na kuweka kumbukumbu kubwa kwa watanzania

Pia amewapongeza wanasingida kwa namna walivyojitoa hadi kupelekea Mkoa wa Singida kwa ujumla na halmashauri ya Ikungi kufanya vizuri katika mbio za mwenge kikanda kwa kushika nafasi ya kwanza nq kuuhehimisha mkoa wa Singida kitaifa

Ikiwa ni mara ya nne kwa Mwenge wa Uhuru kuplekwa mlima Kilimanjaro toka mwaka 1961,Mwaka huu Rais Samia Suluhu Hasan aliagiza mwenge wa uhuru upelekwe mlima Kilimajanro kutokana na sababu mbalimbali ambazo ni pamoja,Mwenge wa uhuru kutimiza miaka 60 toka kuanza kwa mbio zake ,kusherekea miaka 60 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar,Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Miaka 60 ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Miaka 25 ya kumbukizi ya kifo cha baba wa taifa

Bendera ya Taifa na Mwenge wa Uhuru vitapandishwa kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro na Kikosi maalumu cha Makamanda wa JWTZ kikiongozwa na Luten Kanali Halid Hamis Hali

"Tudumishe Michezo na Tuenzi Tamaduni zetu"

Haya yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe Halima Dendego wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Singida (Solya Girls) tarehe 04 oktoba 2024 alipowatembelea Shule hapo

"Mnatakiwa kuhakikisha mnadumisha michezo yote kwani michezo ni afya lakini pia mnaenzi tamaduni zetu za kiafrika

Mjifunze kupika, kufuma, na mengineyo Ili yawasaidie badae na sio kujifunza tuu yaliyopo kwenye vitabu"

Sambamba na Hilo Mhe Dendego amewataka wanafunzi wa Mkoa wa Singida husoma kwa bidii kila mmoja kwa alichochagua kusoma Ili kutimiza malengo yake

"Hakikisheni mnasoma kwa bidii kila mmoja anachosoma lakini kwa kushirikiana na kusaidiana Ili kufikia na kutimiza malengo yake na hatimae Taifa kupata watu makini na wazalendo wa kuliongoza na kulisaidia Taifa hili"

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe Halima Dendego pia amepata chakula cha pamoja na wanafunzi hao wa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Solya

Katika picha ni mkuu wa mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego akimkabidhi cheti mkandarasi wa ujenzi wa jingo la Taaluma litakalogharimu bil. 13.5 katika chuo cha Uhasibu kampasi ya Singida sambamba na kukata Utepe ishara ya kuzindua ujenzi huo

Wanafunzi waaswa kuepuka tabia hatarishi, watakiwa kutumia muda vyema kujisomea kupata maarifa

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mh. Halima Dendego amewataka wanafunzi wa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu kutumia muda walionao sasa kutafuta maarifa ili waje kuijenga Tanzania

Amesema hayo kwenye hotuba yake aliyoitoa Octoba 15, 2024 kwenye ukumbi wa mikutano uliopo katika Chuo cha Uhasibu Singida akiwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa kampeni ya "tuwaambie kabla hawajaharibiwa" Mkoa wa Singida

Aidha Dendego amesema kuwa maarifa hayo watayapata kwenye shule na vyuo wanavyosomea kupitia walimu wao huku akiwataka kusoma kwa bididii na kuachana na kujihusisha na matumazi dawa za kulevya, na vitendo vingine ambavyo ni kinyume na maadili ya Mtanzania

"Tunawategemea, ninyi ndiyo akinababa, Baba ni kichwa na sisi ni mwili, mkiuacha ubaba wenu mnaangamiza Taifa" amesema Dendego

Hata hivyo Dendego amewataka wanafunzi hao kushirikiana vyema na Jeshi la Polisi kitengo cha Dawati la Jinsia katika kupinga ukatili wa kijinsia kwa kutoa taarifa zitakazosaidia kuwabaini wahusika ambapo watakamatwa na sheria kuchukua mkondo wake

Katika hatua nyingine, amelipongeza Jeshi la Polisi kwa kuaandaa kampeni hiyo ambayo amesema itakuwa msaada Mkubwa katika kutokomeza ukatili wa kijinsia

Naye Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida ACP Mayunga Raphael Mayunga amewaelekeza wanafunzi wanaoanza masomo wakiwemo wanafunzi wa kidato cha kwanza , kidato cha Tano na wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa vyuo vya kati na vyuo vikuu kuhakikisha wanayatii makatazo wanayopewa na wazazi/walezi wanapotoka majumbani kwao kwa sababu hao ndiyo wanaojua uchungu wao

Ametumia nafasi hiyo kuwasihi wawe na marafiki wenye tabia nzuri kuliko kujiingiza katika urafiki ambao unaweza kuwatumbukiza katika matumizi ya dawa za kulevya, ulevi wa pombe, na starehe zingine ambazo zinaweza kuwahamisha kimawazo kutoka kusoma hadi kuingia kwenye maisha magumu

RC Dendego Azindua Bodi ya Parole Singida

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mheshimiwa Halima Dendego,ameshiriki katika uzinduzi wa Bodi ya Parole katika ofisi za Magereza Mkoa wa Singida

Hafla hiyo imefanyika katika ukumbi wa Ofisi za Magereza Mkoa imehudhuriwa na Katibu Tawala Mkoa wa Singida,Dkt.Fatuma R.Mganga,wajumbe wa Bodi,Kamati ya Ulinzi na usalama mkoa,Pamoja na Sekretarieti

Akizungumza katika hafla hiyo Mheshimiwa Dendego ameipongeza Bodi ya Parole kwa utendaji mzuri wa kazi huku akisisitiza elimu kutolewa kwa wananchi ili kuelewa kwa undani Zaidi kuhusu majukumu ya Bodi ya Parole na umuhimu wake kwa walengwa wa moja kwa moja ili kuendelea kunufaika na fursa hiyo

Pia, amesisitiza uhamasishaji kwa wazazi kuhakikisha malezi bora ya msingi kwa Watoto wao katika misingi ya dini,mila,desturi na tamaduni kwani kutofanya hivyo kunaongeza idadi kubwa ya vijana wanaojihusisha na uhalifu na baadhi yao wanaomaliza vifungo vyao hudumu uraiani kwa muda mfupi kwani hujikuta wakijiingiza katika vitendo vya uhalifu na kurejea gerezani.

"wazazi warudi katika majukumuyao ya msingi ya kulea Watoto,tusiache nafasi kubwa kwa Watoto kujifunza katika mifumo kama mitandao ya kujamii,bali tuwalee katika misingi ya dini,mila, desturi na tamaduni zetu"Alisema Mheshimiwa Dendego.

Akizungumza katika tukio hilo,Mwenyekiti wa Bodi ya Parole mkoani Singida,Liana A.Hassan ameahidi kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ,Menejimenti Katibu wa Bodi na timu yake katika kutekeleza kazi huku akisisitiza utayari katika kufanya kazi na na ushirikiano baina yao kwa maslahi mapana ya Jeshi la Magereza na Taifa kwa ujumla.

"Tutatoa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa kazi hii ambayo tumeaminiwa kuifanya,tuwe na utayari kufanya kazi ambayo Serikali yetu imetuamini kuifanya"Alisema Liana

Katibu wa Bodi hiyo ambaye pia ni Mkuu wa Magereza Mkoa Singida SACP Khatibu Juma Semzono akizungumza katika uzinduzi huo,amefafanua maana ya Parole kama utaratibu wa sheria unaotoa fursa kwa wafungwa waliofungwa kuanzia miaka minne waliokwisha kutumikia theluthi ya kifungo chao na kuonyesha uelekeo wa kurekebika na tabia nzuri kurudi katika jamii kwa masharti maalumu na kanuni.

Wananchi Manyoni kunufaika na Minara ya Teknolojia ya 4g

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,-Jerry Silaa,amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuhakikisha anaupandisha hadhi mnara uliojenga katika kijiji cha Hika kata Makuru wilayani Manyoni ili wananchi waweze kupata mtandao wa intaneti wa 3G hadi 4G

Ametoa agizo hilo leo wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Hika katika siku ya kwanza ya ziara yake ya siku tano mkoani Singida baaada ya kuzindua mnara wa mawasiliano ya simu uliojengwa na serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) uliojengwa kwa Sh.milioni 272

"Kati ya maelekezo aliyonipa Rais wakati akiniapisha ni kuhakikisha wananchi wanapata mawasiliano, namwelekeza Katibu Mkuu ahakikishe kwa haraka sana mnara huu unapandishwa hadhi na unapata mtandao wa 3G na 4G ili wananchi nao waweze kupata intaneti," alisema

Naye Meneja wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL),Agustino Mwakyembe amesema ujenzi wa mnara huo wenye urefu wa mita 60 ulianza kufuatia kusainiwa kwa makubaliano Machi 16, 2021 na ujenzi wake kukamilika Juni 15, 2022

Amesema mradi huo wenye thamani ya Sh.milioni 272 unatumia teknolojia ya 2G ambao unawezesha wananchi kupiga na kupokea simu za sauti huku wakitumia ujumbe mfupi kwa wakati mmoja (sms)

"Kama sehemu ya dhamira yetu ya kimkakati ya kuimarisha muunganisho katika maeneo ya vijijini tunafanya uboreshaji mkubwa wa minara ya mawasiliano inayofanya kazi sasa kwenye teknolojia ya 2G hadi 4G," alisema

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amesema uzinduzi wa mnara huo ni muhimu sana katika kata ya Makuru na Wilaya ya Manyoni katika kukuza maendeleo na upatikanaji wa huduma muhimu kama vile elimu,afya na biashara na hivyo kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi

Dendego amemuahidi Waziri kuwa umeme utafikishwa katika mnara huo ili uendelee kufanya kazi kwa ufanisi huku wananchi zaidi ya 24,000 wa kata hiyo wakitegemea kunufaika

SINGIDA YA VIWANDA UHAKIKA WA AJIRA NA SOKO LA ALIZETI

Ajira zaidi ya 190 za moja kwa moja na ajira 400 zisizo za moja kwa moja zinatarajiwa kunufaisha wakazi wa Mkoa wa Singida huku wakulima zaidi ya 26000 kunufaika na mradi wa kiwanda cha mafuta cha Wild Flower Grains&Oil Mill Company Limited kupitia uwekezaji mkubwa wa kimkakati uliokamilika kwa asilimia 95 mpaka sasa

Mhe.Jerry Silaa Waziri wa habari na mawasiliano na teknolojia ya habari,alipotembelea kiwanda hicho leo hii amesema ni wakati sasa wa Tanzania kupunguza kuagiza bidhaa nje ya nchi kwani maendeleo ya viwanda yatarahisiaha uchakataji,na upatikanaji wa bidhaa mbali mbali ikiwemo mafuta ya kupikia ambayo yatainua maisha ya wengi katika mchakato wa kupata malighafi kutoka kwa wakulima wa mazao,wasafirishaji mazao,na wauzaji wa bidhaa za kiwandani

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego amewakaribisha wawekezaji kuwekeza katika Mkoa wa Singida kwani ni mahali salama na upatikanaji wa umeme na mazao ya biashara kama alizeti na vitunguu

Amesisitiza wawekezaji wa ndani kujitokeza kayika kuwekeza katika fursa hizo za biashara kwa kuiga mfano wa wawekezaji wazawa wa kiwanda hocho cha mafuta kwani wamethubutu na wameweza kuifanya Singida kupiga hatua katika maendeleo ya viwanda

"Wawekezaji wa ndani waje kujifunza hapa kwetu Singida kwani wataalam wetu wote katika kiwanda hiki kuanzia ujenzi wa msingi wa kiwanda hiki ni vijana wetu wazawa wa hapa hapa Tanzania wakitengeneza bidhaa na kuendesha mashine"

Akiwasilisha taarifa ya mradi wa kiwanda hicho cha mafuta Jamal Shaban,amesema kuwa mipango ya baadae ya kiwanda hicho ni kufanya utanuzi wa kiwanda na kuongeza mashine za kusaga mahindi ili kupata unga

Ujenzi wa shule ya SEKOUTOURE wapunguza msongamano wa wanafunzi Ilongero

Waziri Habari, Mawasiliano na Teknilojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa ameweka jiwe la msingi Shule Mpya ya Sekondari Sekoutoure iloyopo Kata ya Ilongero Wilaya ya Singida kuashiria uzinduzi rasmi wa shule hiyo ambayo ujenzi wake umegharimu kiasi cha zaidi ya Shilingi bilioni moja

Shule hiyo mpya iliyojengwa ililenga kupunguza msongamano mkubwa wa wanafunzi katika shule ya sekondari Ilongero na kuwapunguzia adha wanafunzi kutembea umbali mrefu baadhi ya wanafunzi waliokua wakisoma shule ya Sekondari Ilongero imezinduliwa rasmi leo Oktoba 25, 2024

Akizungumza maara baada ya kukagua majengo na kuweka jiwe la msingi katika shule hiyo Waziri Silaa amesema hiyo ni sehemu tu ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali katika sekta ya elimu nchi nzima ikiwa ni pamoja na Mkoa wa singida

Ametoa rai kwa wanafunzi wa shule hiyo mpya iliyoanza rasmi januari 2023 ikiwa na idadi ya wanafunzi 483 hadi sasa kuhakikisha wanasoma kwa bidii kwa kuwa tayari Serikali imeweka miundombinu bora katika shule hiyo

Akitoa taarifa ya Mradi wa shule hiyo Mkuu wa Shule ya Sekondary Sekoutoure Tatu Njaku amesema ujenzi wa shule hiyo umeboresha mazingira ya Kufundishia na wanafunzi kujifunza

Mkuu wa Mkoa wa Singida Halima Dendego kwa ujumla wake amesema kwa kipindi cha miaka Mitatu ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, Mkoa wa Singida unashule mpya za sekondari 33 ikiwa ni kuendelea kupunguza changamoto za wanafunzi kusoma umbali mrefu

Mikoa ya SIMIYU na ARUSHA kunufaika na ujenzi wa barabara SINGIDA

Ukamilishwaji wa mradi wa ujenzi wa barabara wilayani Iramba kwa kiwango cha lami unategemewa kuwa chachu ya maendeleo kati ya Mikoa ya Arusha, Simiyu na Mkoa wa Singida katika nyanja zote za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla kufuatia Ujenzi wa barabara ya Kitukutu-Gumanga-Chemchem-Sibiti,sehemu ya kitukutu -Kinampanda yenye urefu wa kilometac7.7 kwa kiwango cha lami.

Akizungumza wakati akikagua mradi huo unaofadhiliwa kwa asilimia mia moja na serikali ya TanzaniaWaziri wa habari,mawasiliano na teknolojia ya habari,Mhe. Jerry Silaa, amesema ni wakati wa wakulima na wafanyabiashara kujibu kiu yao ya kupata masoko ya kuuza bidhaa zao zaufugaji, kilimo ikiwemo mahindi,alizeti,pamba na vitunguu pamoja na na biashara nyinginezo

Mhe.Silaa amesisitiza kuwa utekelezaji wa mradi huo utarahisisha upatikanaji na ufikiwaji rahisi wa huduma za afya kwa wananchi wa mikoa hio kwa wakati wote kutokana na miundombinu bora ya barabara hiyo inayotarajiwa kukamilika Machi 2025 na sasa utekelezaji wake ukiwa asilimia 62.5

"Barabara hii inakwenda kukata kiu ya watanzania kutoka Maswa,Mkalama,-Karatu na Meatu kuunganika na Wilaya ya mkalama,Iramba na maeneo mengine.Ni wakati wa wakulima kutumia vizuri ruzuku za pembejeo za kilimo na upatikanaji rahisi wa bidhaa zao za kilimo na ufugaji.alisema Mhe. Silaa

Mradi huo unagharimu kiasi cha Tsh 9.31bilioni ukitekelezwa na mkandarasi mzawa M/s Samota wa Tabora chini ya usimamizi wa TANROADS Singida ukihusisha kunyanyua tuta,tabaka la udongo mgumu,tabaka la simenti,tabaka la kokoto na mwishowe tabaka la lami nyepesi.

Waziri Silaa Atembelea na Kuzindua Miradi ya Zaidi ya Milioni 938 Ikungi, Singida

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Kerry William Silaa (Mb.) amehitimisha ziara yake ya kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo mkoani Singida, akizuru wilaya ya Ikungi. Akiwa huko, alizindua mradi wa maji katika kijiji cha Mnang'ana, uliogharimu zaidi ya shilingi milioni 380 na utahudumia wakazi wapatao 3,000

Waziri Silaa pia alizindua shule ya sekondari ya Puma, iliyogharimu milioni 106.4, ikijumuisha madarasa manne na matundu 8 ya vyoo na kuongeza uwezo wa kuchukua wanafunzi kutoka 80 hadi 160

Aidha, alitembelea jengo la huduma ya mama na mtoto katika hospitali ya wilaya ya Ikungi, ambayo ujenzi wake umegharimu zaidi ya bilioni 2.7

Ziara hiyo ilihitimishwa na mkutano na viongozi na watumishi wa mkoa, ambapo Waziri Silaa alimhakikishia Rais Samia kuwa fedha nyingi zimewezesha maendeleo makubwa katika mkoa huo.

Wananchi Manyoni mbioni kunufaika na mradi wa maji

Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Jerry Silaa ametembea mradi wa maji unaotekelezwa katika mji wa Manyoni mkoani Singida unaotarajiwa kugharimu Sh. 29 Bilioni ukitarajiwa kuwahudumia zaidi ya wananchi elfu 64 katika kata ya Mkwese, Muhalala, na Manyoni mjini

Silaa amewataka watendaji wanaotekeleza mradi meradi huo kuhakikisha unakamilika kwa Wakati Kulingana na thamani ya fedha iliokusudiwa huku akiwasisitiza Kutunza Mazingira na kuwa mradi huo utakapokamilika utakuwa na manufaa wa kazi wenzi wa mji wa Manyoni

Hayo yamejiri katika Halmashauri ya Manyoni mkoani Singida wakati akiwa katika ziara ya siku 5 mkoani humo ya kukagua, kuzindua na kutembelea miradi Mbalimbali ya mawasiliano na miradi mingine ya Kimaendeleo

"kazi hii ndio matokeo ya fedha ambazo tumekuwa tukizisema Wakati wote ambao Mheshimiwa Rais amekuwa akizileta kwaajili ya miradi ya Maendeleo, kwahiyo niwatie shime watendaji katika mradi huu wahakikishe unakamlika kwa Wakati kutokana na fedha na wananchi tuendelee kuitunza miradi hii kwa manufaa yao" alisema

Mkuu wa mkoa wa Singida Mhe, Halima Dendego ameishukuru serikali kwa uwezeshaji wa mradi huo na kwamba utakapokamilika utasaidi sana katika kutatua changamoto ya maji na kumaliza Maswali ya wananchi ya kuwa mradi unakamilika lini

"Tumeshatembelea sana hapa lakini tunashukuru kwa msaada wa serikali hii mana tunaenda kupata maji ndani ya muda mfupi"

Kwa mujibu wa mkuu wa wilaya ya Manyoni Vincent Bashinji katika taarifa yake, mradi huo mpaka sasa umefikia asilimia 30 za utekelezaji wake huku vijana zaidi 85 wakipata ajira kutokana na mradi huo na kuchochea ukuaji wa uchumi katika eneo hilo

Aidha waziri silaa ametembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule ya msingi Mlowa iliopo halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni wenye thamani ya zaidi ya sh. 493 milioni

Uvamizi wa Tembo Ikungi wapatiwa mwarobaini wake

Kufuatia uvamizi wa tembo katika kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi,Waziri wa Maliasili na Utalii,Mhe. Balozi, Dkt. Pindi Chana (Mb) ameelekeza timu ya Askari Uhifadhi 18 kuweka kambi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Mkoani Singida kwa lengo la kukabiliana na tembo wanaovambia makazi ya watu.

Akizungumza na wananchi katika Mkutano wa hadhara Oktoba 28,2024 kwenye Kijiji cha Mkiwa Wilaya ya Ikungi, Mkoani Singida Mhe. Chana amesema nia ya Serikali ni kuhakikisha changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo inapungua au kumalizika kabisa.

"Tunakwenda kuongeza askari watakaotusaidia kuhakikisha tembo wanarudi katika maeneo yao ya hifadhi sambamba na kuongeza mabomu baridi kufukuza tembo" Mhe. Chana amesisitiza.

Aidha, amesema Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji,Wilaya na Mkoa itafanya zoezi la kutambua na kuweka alama katika maeneo ya Korido za wanyamapori (shoroba) na kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutoweka shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo.

"Baada ya kuzitambua shoroba tunataka kuwepo na shughuli za uhifadhi mfano kuanzisha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) ili kuendeleza uhifadhi" Mhe. Chana amesisitiza

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego amewataka wananchi wa Ikungi kutoa ushirikiano kwa Askari Uhifadhi hao ili kukabiliana na tembo ipasavyo ikiwemo kwa wahitimu wa jeshi la akiba kupata mafunzo maalum juuvya kukabiliana na tembo ili kuwa msaada pale ambapo tembo watajitokeza

NMB yaja na mikakati ya kukuza huduma za kifedha Singida

Kufuatia muendelezo wa wiki ya huduma kwa wateja,Viongozi na watumishi wa Bank ya NMB wametembelea ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida kwa lengo la kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi popote pale walipo.

Mkuu wa mkoa wa Singida,Mhe. Halima Dendego akizungumza katika hafla hiyo amesema ni wakati wa Mkoa wa Singida kukua katika matumizi ya huduma za kibenki kwa kuboresha na kuwafikia wananchi wengi zaidi katika huduma za kibenki hususani kwa wananchi wa vijijini katika maeneo ya uzalishaji hivyo ni wakati wa kufanya utafiti ili kigundua maeneo ya uzalishaji na yenye mzunguko mkubwa wa kifedha ili kupeleka huduma maeneo hayo kwa kuongeza idadi ya mawakala na mashine za ATM.

Dendego amesema Kwa kufanya hivyo,uzalishaji utaongezeka maradufu kutokana na upatikanaji na mzunguko wa fedha kuwa rahisi na usalama wa wananchi utaongezeka kwani wataepuka kuhifadhi ela ndani na kutumia njia rahisi za kibenki katika utunzaji wa fedha zao.

"Ni vyema tuainishe maeneo mbali mbali yanayohitaji kufikiwa na huduma za kifedha mjini na vijijini ili kupeleka huduma karibu na wananchi kwa lengo la kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla kwani mzunguko wa fedha utakua mkubwa na uzalishaji utaongezeka"alisema Dendego.

Katibu tawala Mkoa wa Singida,-Daktari Fatuma Mganga,amesema ni wakati wa wananchi kunufaika na huduma za kibenki hususani kwa wananchi wa vijijini wanaojishughulisha na uzalishaji kwa kufunguliwa akaunti na kupewa elimu juu ya matumizi ya huduma za kibenki.

Pia amesisitiza elimu ya huduma hizo kutolewa katika vikundi mbali mbali ikiwemo vikundi vya wanawake, vikundi vya mikopo ya Halmashauri ,wakulima na wafanyabiashara ili kuwapa utayari wa kuthubutu kutumia huduma za kibenki zenye gharama nafuu na usalama wa kutosha.

Naye Meneja wa Benki ya NMB mkoani Singida,ameahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa kuhakikisha wanayafikia maeneo yote ya Mkoa wa Singida katika kuhakikisha wanafikiwa na huduma za kifedha mahali popote na wakati wowote kwa kuongeza idadi ya mawakala wakubwa mjini na vijijini pia uwepo wa ATM zitakazorahisisha upatikanaji wa fedha zaidi.

Sekretarieti ya Mkoa wa Singida yatengeneza mpangokazi wa Taasisi

Wajumbe wa sekretarieti ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida wameshiriki katika kuandaa mpango kazi wa ofisi hiyo kuanzia Oktoba Mosi,2024 ambapo yalifunguliwa rasmi na Mkuu wa Mkoa Mhe.Halima Dendego na Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Daktari Fatuma Mganga huku mkufunzi akiwa Daktari Titus Mwageni kutoka Chuo cha Mipango Dodoma.

Akizungumza siku ya ufunguzi,Mkuu wa Mkoa Halima Dendego amesema ana matumaini makubwa kuwa mpangokazi wa ofisi hiyo utamamilika na kuleta mageuzi makubwa katika utendaji kazi wa taasisi kwa kila mtumishi,vitengo na idara kufanya majukumu yao vyema na kwa weledi

"Kukamilika kwa mpangokazi kutachochea utendaji kazi bora katika taasisi yetu kwawatymishi wote kuyatambua majukumu yao na kuyafanya kwa weledi,hivyo tushirikiane kwa pamoja kutekeleza jambo hili kwa maslahi mapana ya Sekretarieti ya Mkla wa Singida."alisema Mhe.Dendego.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida,Daktari Fatuma Mganga ametoa rai kwa watumishi hao kuungana kwa pamoja kuhakikisha mpangokazi wa taasisi unapatikana ambao utaakisi yake yote yatakayotendeka katika Ofisi hiyo kwani ni chachu ya utendaji bora wa kazi kuanzia ngazi ya kitengo,idara na Mkoa kwa ujumla.

Akizungumza baada ya maandalizi ya mpangokazi wa taasisi,Baraka Mhembano ambaye ni Afisa Tehama kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida amefurahishwa na mafunzo hayo yaliyosaidia upatikanaji wa mpangokazi huo akisema kuwa licha ya kupatikana kwa mpango huo wamejifunza mengi yaliyowajenga vizuri katika uzoefu wa mazingira ya kazi na namna ya kutatua changamoto mbali mbali.

LIMEANDALIWA NA:
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Kitengo cha Habari na mawasiliano
S.L.P. 05
Singida

Kwa maoni na ushauri wasiliana nasi kupitia
Simu: 026 250 2089/2249
Fax: 026 250 2078
E-mail: ras@singida.go.tz
info@singida.go.tz

Endelea kutufuatilia kwenye kurasa zetu